

**Jibu:** Turejee..

*1Nyakati 28:17 “na nyuma, na mabakuli, na vikombe vya dhahabu safi; na kwa MATASA ya dhahabu, kwa uzani kwa kila TASA; na kwa matasa ya fedha, kwa uzani kwa kila tasa”.*

Ukisoma kuanzia juu utaona kuwa hivyo ni vyombo ambavyo vingepaswa viwepo ndani ya MUNGU aliyokusudia kuijenga Mfalme Daudi.

Lakini kwasababu haikuwa mapenzi ya MUNGU mfalme Daudi aijenge ile nyumba bali mwanae (*Sulemani*)...hivyo ilimbidi Mfalme Daudi ampe maelekezo ya namna ya kuijenga ile nyumba na viwango vyake.

Moja ya maagizo aliyompa kulingana na alivyooneshwa na Bwana ni uwepo wa MATASA ndani ya nyumba hiyo..*(kwamba atakapojenga basi aweke Matasa ya dhahahu ndani yake).*

### **Sasa Matasa yalikuwa ni nini?**

Matasa yalikuwa ni “**Makarai/mabeseni**” ya dhahabu yaliyowekwa ndani ya Hekalu kwa kusudi la kutawadha (*kunawa*).

Kwasababu ndani ya Hekalu kulikuwa na makuhani wengi waliokuwa wanafanya kazi mbalimbali na kwa zamu, na kulingana na desturi za wayahudi ilikuwa ni lazima kila Kuhani anawe

*(atawadhe)* kabla ya kuanza kazi ya kikuhani na hata baada ya kumaliza.

Hivyo vyombo hivyo (MATASA) vilitumika kuhifadhia maji kwaajili ya shughuli hiyo.

Na pia vilikuwepo **VITASA** hivi vilikuwa ni vibaluli vidogo vya kuweza kushikwa kwa mkono, tofauti na Matasa ambayo yalikuwa yanabeba ujazo mkubwa wa maji, na vitasa ndio vile vinavyotajwa katika kitabu cha Ufunuo wa *Yohana mlango wa 15 na 16*.

*Ufunuo 15:5 “Na baada ya hayo nikaona, na hekalu la hema ya ushuhuda mbinguni lilifunguliwa;*

*6 na wale malaika saba, wenye mapigo saba, wakatoka katika hekalu, wamevikwa mavazi ya kitani safi, ya kung’aa, wamefungwa vifuani mwao mishipi ya dhahabu*

*7 Na mmoja wa wale wenye uhai wanne akawapa wale malaika saba VITASA SABA vya dhahabu, vimejaa ghadhabu ya Mungu, aliye hai hata milele na milele”.*

## **Ni nini tunajifunza katika hayo?**

Tunachoweza kujifunza ni kuwa matasa ya Hekalu la duniani yalijaa maji ya kuoshea makuhani lakini vile VITASA vya Hekalu la mbinguni vimejaa hasira na hukumu ya MUNGU kwa wanadamu wasiomcha yeye.

Bwana atusaidie tumtafute, tusipotee wala kuangukia katika hukumu yake.

Maran atha.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

### **Mafundisho mengine:**

**[Kile kinara cha Taa ndani ya Hekalu la Sulemani kilikuwa kinawakilisha nini?](#)**

**[Sanduku la Agano lilikuwa linawakilisha nini katika Agano jipya?](#)**

**[YAKINI NA BOAZI.](#)**

**Je wakati Bwana YESU anazaliwa shetani alikuwa amefungwa?**

**Vihekalu vya fedha vya Artemi vilikuwaje? (Matendo 19:24).**

**Rudi Nyumbani**

Share on:  
WhatsApp